



**MAELEZO YA BRIGEDIA JENERALI JOHN JULIUS MBUNGO  
MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU WAKATI WA HAFLA  
YA UREJESHAJI WA FEDHA ZA USHIRIKA KWA  
WANANCHI MKOANI NJOMBE AGOSTI 17, 2020**

**Mhe. Suleiman Jafo**

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali  
za Mitaa;**

**Mhe. Eng. Mwita Marwa Rubirya**

**Mkuu wa Mkoa wa Njombe**

**Mhe. Katarina Revocati**

**Katibu Tawala wa Mkoa,**

**Kamati ya Ulinzi ya Mkoa wa Njombe,**

**Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Njombe,**

**Ndugu Wananchi na Waandishi wa Habari;**

Habari za asubuhi, Bwana Yesu Asifiwe, Asalaam Aleykum,  
Tumsifu Yesu Kristo...

**Mhe. Waziri,**

Natumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote afya njema hata tumekutana hapa siku hii ya leo katika tukio hili muhimu la UREJESHAJI WA FEDHA ZILIZOOKOLEWA KATIKA OPERESHENI ZA KUKUSANYA MADENI YA VYAMA VYA USHIRIKA AMCOS.

**Mhe. Waziri,**

Mtakumbuka kwamba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU ilikabidihiwa jukumu la kukusanya madeni sugu pamoja na kurejesha fedha zilizofanyiwa ubadhirifu ambazo ni mali ya Vyama vya Msingi - AMCOS na SACCOS ili fedha hizo zote ziweze kurejeshwa kwa wananchi wanyonge waliोधulumuwa. Jukumu hili tumelitekeleza kikamilifu NCHI NZIMA ambapo kwa ujumla wake tangu tuanze operesheni hii Novemba 2019, tumefanikiwa kukusanya zaidi ya **shilingi Bilioni 16.3.**

**Mhe. Waziri,**

Tunayo furaha kuujulisha umma kwamba kati ya fedha hizo tulizookoa nchi nzima **shs. 5,042,594,589.82 (Bilioni tano, Milioni Arobaini na Mbili, Laki Tano na Tisini na Nne Elfu, Mia Tano na Themanini na Tisa na Senti Themanini na Mbili)** zimeokolewa katika mkoa wa Njombe.

**Mhe. Waziri,**

Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana Viongozi wa mkoa wa Njombe, Wakuu wote wa Mikoa, Warajisi wa Vyama pamoja na Wakuu wa Wilaya kote nchini kwa ushirikiano waliotupatia katika kuhakikisha kuwa Operesheni hii inafanyika kwa ukamilifu na mafanikio makubwa nchi nzima.

Tunawahakikishia wananchi kwamba, TAKUKURU kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Usalama itasimamia zoezi lote la kuhakikishia kuwa fedha hizi zinafikishwa kwa walengwa na tutahakikisha kuwa viongozi wote waliohusika katika ubadhirifu wa fedha hizi ambao waliwakosesha wananchi wanyonge haki zao wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za nchi.

**Vilevile,** natoa ONYO kwa viongozi wote watakaokabidhiwa fedha hizi, kwamba kuanzia sasa wawe makini na watekeleze majukumu yao ya kuwahudumia wananchi wanyonge kwa UADILIFU. Wajifunze kutokana na makosa yaliyotendwa na watangulizi wao, kinyume na hapo wawe tayari **KUNG'ATWA na TAKUKURU.**

**Mhe. Waziri,**

Nitakuwa sijatenda haki kwenu, kwangu na Taasisi ninayoiongoza iwapo nitaondoka hapa bila kuongelea suala muhimu la UCHAGUZI MKUU WA MWAKA HUU 2020.

Nchi yetu inaingia katika zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika Octoba 28, 2020 kote nchini.

Tunafanya Uchaguzi wa namna hii kila baada ya miaka mitano ili kutekeleza matakwa ya kidemokrasia sambamba na kupata viongozi waadilifu watakaoshughulikia na kuyatatua matatizo yanayowahusu ninyi wananchi wanyonge. Kura yako wewe mwananchi ina thamani kubwa sana kwani ndiyo inayompatia kiongozi dhamana ya kuongoza; Bila kura yako hakuna mwenye nafasi ya kupata uongozi.

Ninawaasa wagombea na wapiga kura kote nchini kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Nchi wakati wa Kampeni mpaka baada ya Uchaguzi. Tufanye Kampeni za kistaarabu bila kushiriki katika matendo ya Rushwa yanayodhalilisha UTU wa watanzania.

Ninafafanua tena kwa vyombo vya habari – TAKUKURU inatekeleza majukumu yake bila woga wala upendeleo na bila kujali ni chama gani kinatuhumiwa.

***CHONDE CHONDE WATANZANIA TUSIKUBALI  
KUWACHAGUA VIONGOZI WANA OJIHUSISHA NA  
VITENDO VYA RUSHWA!***

Asanteni sana kwa kunisikiliza;

J.J. MBUNGO, *ndc*  
**BRIGEDIA JENERALI**  
**MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU**